HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

TOLEA LA 007 | SEPTEMBA 2023 | HALIUZWI

Jarida la

# TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI

## TEMEKE YAIBUKA MSHINDI MAONESHO YA SABASABA





**_Lipa Kodi na Tozo kwa maendeleo ya Manispaa yetu._**

MHARIRI MKUU
**FRANCISCA MSELEMU**

WAHARIRI WASAIDIZI
**SWEETBETTER NJIGE**
**SHALUA MPANDA**
**JOANITA JOSEPH**

WAPIGA PICHA
**METHEW JONAS**
**GERVAS EDICK**

MSANIFU WA JARIDA
**MICHOLAX MUSSA**

JARIDA HILI HUTOLEWA NA;
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**
**S. L.P 46343 TEMEKE, DSM.**
**SIMU: +255 22-2928132**
**NUKUSHI: +255 22-2928137**
**BARUA PEPE: temekemc.go.tz**
**TOVUTI: www.temekemc.go.tz**



# TEMEKE YAIBUKA MSHINDI MAONESHO YA SABASABA

**Na** Sweetbetter Njige

Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi tuzo mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndg. Elihuruma Mabelya baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Banda bora kwa halmashauri zilizoshiriki maonesho ya 47 ya biashara (Sabasaba) yaliyofanyika katika viwanja vya Mwl. Nyerere, ofisi za TANTRADE jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla ya kufunga maonesho hayo Dkt. Mwinyi amewataka wafanyabiashara Nchini kuwa waaminifu katika bidhaa wanazotuma kwenda nje ya nchi ili kuendelea kuaminiwa.

Aidha Dkt Mwinyi amewataka wafanyabiashara hapa nchini kutumia maonesho hayo ya kimataifa ya biashara kupata ujuzi na kuboresha biashara zao ili kuweza kupata masoko zaidi nje ya Nchi.
"Wito wangu kwenu wazalishaji na wafanyabiashara hakikisheni mnapopokea oda zenu kutoka nje fanyeni kwa uaminifu mkubwa".Alisema Rais Mwinyi

Dkt.Mwinyi amesema amefurahishwa na maboresho ya miundombinu ya Maonesho hayo ya Biashara zikiwemo barabara za lami ukilinganisha na maonesho ya 46.

Maonesho hayo ya 47 yenye ujumbe unaosema "Tanzania mahali sahihi pa biashara na uwekezaji"yalifunguliwa rasmi Juni 28 mwaka huu na yamefungwa rasmi leo Julai 13.alipata fursa ya kusikiliza changamoto mbalimbali katika utoaji huduma ikiwemo ukosefu wa chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na changamoto nyingine.



# MHE.UMMY MWALIMU ATANGAZA NEEMA TEMEKE

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Waziri wa afya nchini Mhe Ummy Mwalimu amefanya ziara katika manispaa ya Temeke lengo likiwa ni kupokea taarifa ya utoaji wa huduma za afya pamoja na kukagua miradi ya ujenzi.

Ziara hiyo imefanyika leo Agosti 9,2023 ambapo Mhe.Ummy alipokea taarifa ya halmashauri ya manispaa ya temeke hususani katika sekta ya afya pamoja na kutembelea hospitali ya Mbagala Rangi tatu, iliyopo kata ya Mbagala wilayani Temeke ambapo alikagua mradi wa ujenzi wa jengo la ghorofa 6.

Aidha Waziri huyo wa Afya alipata fursa ya kusikiliza changamoto mbalimbali katika utoaji huduma ikiwemo ukosefu wa chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na changamoto nyingine.

Waziri Ummy Mwalimu pia amemtaka mkandarasi kukamilisha jengo hilo kwa wakati ili huduma ziweze kutolewa na kuahidi Serikali itaongeza shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya kuharakisha ujenzi huo.

Mhe Ummy aliongeza kuwa katika kuendelea kuimarisha huduma za afya Serikali itajenga hospitali nyingine ya wilaya ya Temeke pamoja na kupandisha hadhi zahanati 2 kwa kila jimbo kuwa na vituo vya afya.

" Mhe Rais Samia Suluhu Hassan hajatosheka na kuwa na hospitali hii ya Mbagala hivyo amenielekeza niwaelekeze hospitali ya Taifa Muhimbili kutoa ekari 30 pale Vikuruti, Chamazi na kuipatia manispaa ya Temeke kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya". Alisema Mhe. Ummy

Sekta ya Afya katika manispaa ya Temeke imekuwa ikiboreshwa kwa kasi kubwa katika kipindi hiki cha Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.



# RC CHALAMILA AWATAKA WAKUU WA WILAYA DSM KUIGA MFANO TEMEKE

**Na** Shalua Mpanda

Maadhimisho ya Siku ya Usafi Duniani yameadhimishwa leo Septemba 16, 2023, ambapo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Albert Chalamila, alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Zakhiem Mbagala, wilayani Temeke.

Akizungumza katika maadhimisho hayo yaliyoanza kwa matembezi ya mwendopole (jogging) na zoezi la usafi, Mkuu huyo wa Mkoa amepongeza uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Mkuu wa Wilaya kwa kuwa kinara katika kampeni ya usafi mkoani Dar es Salaam.

Mhe. Chalamila amesema katika mkoa wa Dar es salaam Manispaa ya Temeke pekee ndio yenye kampeni kubwa ya usafi na viongozi wake wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya Mhe. Mobhare Matinyi, wamekuwa mstari wa mbele kusimamia usafi.

"Mkuu wa Wilaya na menejimenti yote ya Manispaa Temeke imekuwa na kazi nzuri sana ya kusimamia usafi na nitoe rai na wito kwa wakuu wa wilaya, mameya na wakurugenzi wote wa mkoa wa Dar es Salaam kuiga mfano wa kampeni inayofanywa Temeke," alisema Mhe. Chalamila.

Akimkaribisha Mkuu wa Mkoa kuzungumza na wananchi pamoja na wadau wa usafi, afya na mazingira, Mkuu wa Wilaya Mhe. Matinyi alisema kuwa kwa kuona umuhimu wa usafi wa mazingira wana-Temeke waliamua kuanzisha wiki ya usafi iliyozinduliwa Septemba 11 mwaka huu kwa kufanya shughuli mbalimbali zikiwemo usafishaji wa mitaro, mifereji, masoko na mitaa.

Maadhimisho hayo ya Siku ya Usafi Duniani yamefikia kilele leo hii lakini Mhe. Matinyi ametumia nafasi hiyo kutangaza wiki mbili zaidi za kuendelea na kampeni ya usafi kulenga mitaro na mifereji ili kujiandaa na mvua za El Nino zitakazoanza mwezi Oktoba.



# WAZIRI WA AFYA AWASIHI WATANZANIA KUBADILI MTINDO WA MAISHA

Na Joanita Joseph -TMC Habari

Katika kuadhimisha siku ya Moyo duniani leo Septemba 29, 2023 Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ambaye pia ni mgeni rasmi katika maadhimisho hayo amewasihi watanzania kubadili mtindo wa maisha kwa kuzingatia ulaji bora unaofaa na kufanya mazoezi angalau dakika 150 kwa wiki ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo shinikizo la juu la damu inayopelekea matatizo ya Moyo na mishipa ya fahamu.

Waziri Ummy amebainisha kuwa takwimu zinaonyesha kuwa kuna ongezeko la 9.4% kwa wagonjwa wa moyo lakini pia katika kila watanzania 100, 12 wana kisukari na 25 wana tatizo la shinikizo la damu, hivyo ni vyema wananchi wakazingatia kinga kuliko tiba kwani matibabu ni gharama kubwa.

Vilevile ameongeza kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia wizara ya afya imedhamiria kufanya maboresho makubwa katika sekta ya afya ikiwemo kuweka miundo mbinu ya kisasa ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora.

"Tumepunguza kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi kwa 80% yaani kati ya wagonjwa 10 wawili ndio wanaenda nje lakini kupitia Mama Samia Specialization program Bilioni 9 imetumika kusomesha madaktari bingwa wa moyo " alisema Waziri Ummy

Halkadhalika ametoa wito kwa wananchi kujenga mazoea ya kupima afya zao ili kuanza matibabu mapema pale wanapogundulika na tatizo lakini pia Madaktari wajiendeleze kitaaluma kwani Serikali ipo tayari kugharamia kwa manufaa ya afya za watanzania.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Ya Temeke Mhe. Mobhare Matinyi ambaye amemuwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ametoa pongezi na shukrani za dhati kwa taasisi ya Moyo kuipa heshima siku hiyo na kwa Serikali kwa jinsi inavyoendelea kufanya maboresho na kutoa huduma za kitaalamu hususani katika Sekta ya Afya Nchini.

Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu ya 'Tumia Moyo wako kulinda Moyo wako' yamefanyika katika eneo la Hospital ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dar Group ambapo Wataalamu wa Taasisi ya Moyo kwa kushirikiana na Chama Cha Madaktari bingwa wa Moyo Tanzania (TCS) wataweka kambi maalum kwa siku 2 katika hospital hiyo itakayohusisha upimaji.



# NAIBU WAZIRI NDEJEMBI: TUTAFANYIA KAZI CHANGAMOTO YA UKOSEFU WA MAENEO YA UJENZI WA SHULE TEMEKE

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),mheshimiwa Deogratias Ndejembi amefanya ziara kukagua miradi mbalimbali ya elimu inayotekelezwa wilayani Temeke.

Katika ziara hiyo ya kukagua miradi ya elimu kwa upande wa shule za Msingi na Sekondari,Mhe.Ndejembi amesema halmashauri ya Temeke imekuwa ikipokea fedha nyingi za miradi ya elimu kutoka Serikali kuu ambapo kwa mwaka uliopita ilipokea zaidi ya milioni 400 ila changamoto kubwa ni ufinyu wa maeneo ya ujenzi wa madarasa.

"Tunatambua kuwa kuna changamoto ya maeneo na hili ni tatizo la mkoa mzima wa Dar es salaam ndio maana tunapendekeza ujenzi wa shule za ghorofa na sisi kama Ofisi ya Rais tutakwenda kukaa tuje na michoro maalum kwa ajili ya mkoa wa Dar es salaam na manispaa zake".Alisema Naibu Waziri huyo

Aidha Mhe.Ndejembi amewataka viongozi wa manispaa ya Temeke kukamilisha ujenzi wa shule ya Sekondari Dovya kwa muda waliokubaliana Ili kuwezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza waweze kuyatumia.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri huyo aliongizana na Mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe.Mobhare Matinyi,Meya wa manispaa ya Temeke Mhe.Abdallah Mtinika,waheshimiwa wabunge wa majimbo ya Mbagala(Abdallah Chaurembo) na Temeke(Dorothy Kilave),Mkurugenzi wa Manispaa hii ndugu Elihuruma Mabelya na viongozi wengine wakiwemo wa Chama Tawala(CCM).



# RC CHALAMILA AWATAKA WANANCHI KUHESHIMU TAALUMA YA UDAKTARI

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam mheshimiwa Albert Chalamila amezindua kampeni ya utoaji wa huduma za afya bure(Afya check) mkoa wa Dar es salaam na kuwataka wananchi kuheshimu taaluma ya udaktari.

Akiwa katika uzinduzi wa kampeni hiyo kimkoa iliyofanyika katika viwanja vya Shule ya msingi Mbagala Rangitatu,Mhe.Chalamila amewaasa wananchi kutokuchezea kada hiyo kwa kuwa inagusa moja kwa moja uhai wa binadamu.

Mkuu huyo wa Mkoa amegusia kipande cha video fupi kilichosambaa mitandaoni kikimuonesha mmoja wa wauguzi akisafisha vifaa vya hospitali na kuvianika juani na kusema kitendo hicho si sawa lakini pia si sahihi kumuona mwenzako akipata matatizo kazini.

"Tusifurahie sana mimi mkuu wa Mkoa nikaja hapa nifanye maamuzi kuwa daktari huyu aondoke,itafika kipindi mtoto wako ataumwa na mimi sio daktari,mtoto wako atakufa...ukiona kuna mtumishi wa afya amekosea,fuata viongozi waeleze watakaa nae waongee ikishindikana mwisho ndio ifike hatua ya kufukuzana".Alisema Mkuu huyo wa Mkoa

Kampeni hiyo ya utoaji wa huduma Bure za afya ulioratibiwa na wadau mbalimbali wakiwemo kipindi cha Afya Check kinachoongozwa na Dkt Isaac Maro, imezinduliwa kimkoa leo ambapo jumla ya watu elfu 20 wanatarajiwa kupatiwa matibabu na vipimo vya afya bure katika mkoa huu wa Dar es salaam



# WAMACHINGA MBAGALA KUPANGIWA MITAA MAALUM YA KUFANYIA BIASHARA

**Na** Shalua Mpanda

Uongozi wa wilaya ya Temeke umepanga mitaa maalumu ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara ndogondogo(wamachinga) wanaofanya shughuli zao maeneo yasiyo rasmi hasa katika eneo la Mbagala Rangitatu.

Hayo yamebainishwa na mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mobhare Matinyi alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao Septemba 21,2023.

Mhe.Matinyi amesema nia ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe.Rais Dkt Samia Suluhu ni kuona Wananchi wanaongeza kipato kwa kujishughulisha na biashara lakini pia usalama wao kulindwa kwa kufanya shughuli zao maeneo ambayo sio hatarishi.

Amesema Serikali imetoa fedha nyingi kutengeneza barabara za mitaa kwenye Wilaya hii kwa lami na zege ambayo uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na viongozi wa wafanyabiashara hao wanaweka utaratibu wa kuwahamishia huko.

"Pamoja na uhalali wa kufanya biashara,lakini si uungwana wala si haki kufanya biashara katika eneo la barabara...viongozi wenu wanaendelea kuwasajili Ili kuwahamishia kwenye mitaa tuliyoipanga".Alisema Mhe.Matinyi

Kwa upande wake mwenyekiti wa wafanyabiashara hao Bw.Hashim Joram amemuhakikishia Mkuu wa wilaya kuwa ifikapo kesho zoezi la kuwasajili litakuwa limekamilika na mwisho wa mwezi huu wafanyabiashara wote watakuwa kwenye maeneo yaliyopangwa.

"Usajili unaendelea na leo tumefanya upande huu wa darajani,kesho tunahama upande wa pili na mpaka sasa timeshasajili wafanyabiashara 269,kesho wote hawa tunaenda kwenye mitaa yetu kugawana maeneo".Alisema Mwenyekiti huyo

Eneo hilo la Mbagala limekuwa na mkusanyiko mkubwa wa wafanyabiashara hao ambao wamekuwa wakifanya biashara zao hali ambayo inasababisha uchafuzi wa Mazingira hayo na kuhatarisha usalama wao kwa kupanga bidhaa kwenye barabara hiyo.




# MEYA MTINIKA AFUNGUA MKUTANO WA WADAU WA MAZINGIRA KUTOKA NCHI 12 DUNIANI

**Na** Shalua Mpanda

Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Abdallah Mtinika leo Septemba 28,2023 amefungua mkutano wa wadau wa Mazingira kutoka nchi 12 duniani.

Mkutano huo ulioandaliwa na taasisi ya Tomorrow 's Cities,UCL kutoka Uingereza una lengo la kuzibaini changamoto mbalimbali zinazosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Katika hotuba yake ya ufunguzi Mhe.Mtinika amesema uharibifu wa mazingira na ujenzi usiofuata utaratibu umekuwa chanzo kikubwa cha mafuriko katika maeneo mengi mkoani Dar es salaam na hasa katika wilaya ya Temeke.

"Ninaishukuru sana taasisi hii ya Tomorrow 's Cities kutoka Uingereza na Chuo Kikuu cha Ardhi kwa kuchagua wilaya Temeke kufanya mkutano huu,hii ni faraja kwetu".Alisema Mhe.Mtinika.

Mwakilishi kutoka Taasisi hiyo Bw.Mark Pelling amewaeleza washiriki wa mkutano huo kuwa wanahitaji nguvu ya pamoja kuweza kupambana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi.

Baadhi ya wawakilishi kutoka nchi mbalimbali waliohudhuria mkutano huo waliweza kuelezea jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali zao na taasisi nyingine kuweza kukabiliana na changamoto hii.

Jumla ya Nchi 12 zikiwemo Gambia,Zimbabwe,Kenya,Uganda,Afrika ya Kusaini,Uingereza, Morocco zimeshiriki Mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Idd Nyundo uliopo katika ofisi za manispaa ya Temeke.



# WADAU NA WATAALAM WA KIMATAIFA KUIPA TEMEKE MBINU ZA KUKABILIANA NA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI

**Na** Shalua Mpanda

Manispaa ya Temeke inaendelea kuchukua tahadhari dhidi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambapo Mstahiki meya Abdallah Mtinika amekutana na wataalamu wa Taasisi ya Tomorrow 's Cities kutoka Uingereza.

Lengo la kikao hicho ni kuweka mikakati na kujenga uelewa wa namna jinsi ya kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yakiwemo mafuriko yanayoweza kusababishwa na mvua za El-nino zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mtinika amesema wanatarajia kufanya kikao kikubwa Septemba 28 mwaka huu ambapo wawakilishi wengine kutoka nchi mbalimbali watashiriki.

"Lengo kuu la mkutano huu ni kufanya Utafiti utakaosaidia wanatemeke kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi hasa mafuriko na pia upangaji wa miji".Alisema Meya Mtinika

Taasisi hiyo ya Tomorrow 's Cities itafanya Utafiti huo kwa kipindi cha miezi 6 ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es salaam anbapo itabaini changamoto zote zinazosababisha mafuriko katika baadhi ya maeneo.

Kwa upande wake mtaalam kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es salaam Profesa Willbard Kombe amesema umuhimu wa Utafiti huu ni kwamba utasaidia kutambua ukubwa wa maafa na namna ya kuweza kukabiliana na maafa hayo.

Mwakilishi kutoka taasisi ya Tomorrow 's Cities UCL,Bw.Mark Pelling amemshukuru Meya Mtinika kwa kuwaalika kufanya Utafiti huo katika wilaya ya Temeke na kusema kuwa Utafiti huu utaleta matokeo chanya na kuweza kukabiliana na majanga yanayoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkutano huu wa ufunguzi pia umewakutanisha maafisa Ardhi na mipango miji kutoka manispaa ya Temeke pamoja wataalamu wengine.



# IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA YAENDESHA MAFUNZO KWA WATENDAJI SERIKALI ZA MITAA TEMEKE

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Viongozi wa mitaa wilayani Temeke wamepata semina ya mafunzo kuhusu Sheria zinazohusika na Utawala wa Serikali za Mitaa,kusimamia maadili,Usafi na taka ngumu,Sheria ya 6%,vibali vya ujenzi,leseni za Biashara pamoja na usimamizi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo

Semina hii imefanyika shule ya Sekondari Jitegemee ambapo inatarajiwa kufunguliwa rasmi na Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mhe.Abdallah Mtinika.



# WAJUMBE KAMATI YA FEDHA WAFANYA ZIARA UKAGUZI WA MIRADI

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Wajumbe wa Kamati ya Fedha wa Baraza la madiwani pamoja na wataalamu kutoka manispaa ya Temeke leo hii Agosti mosi 2023 wamefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Miongoni mwa Miradi hiyo ni ujenzi wa shule mpya ya msingi mchepuo wa kiingereza Mikwambe iliyopo kata ya Toangoma ambapo ujenzi wake umefikia hatua ya kunyanyua kuta.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo diwani wa kata ya Mtoni ambaye pia ni mjumbe wa Kamati hiyo ya Fedha mheshimiwa Amina Batash amemshukuru Mhe.Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha wanapata shule yenye hadhi hiyo ambayo itakuwa msaada mkubwa kwa Manispaa hii kwa upande wa kuinua ufaulu na elimu kwa ujumla.

Kwa upande wake Naibu Meya wa manispaa ya Temeke Mhe.Arnold Peter amesisitiza ushirikiano katika utekelezaji wa miradi hii ili iweze kukamilika kwa wakati na wananchi wapate huduma huku akiwataka watumishi kufanya kazi kwa weledi na kwa mujibu wa miongozo na taratibu za utumishi wa Umma.

Manispaa ya Temeke ni moja ya manispaa nchini ambazo zinatekeleza miradi mingi ya elimu kutokana na fedha za makusanyo ya ndani na nyingine kutoka Serikali kuu ili kuweza kukidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi katika wilaya hii yenye idadi kubwa ya wakazi hapa nchini.



# TEMEKE YAFANYA KIKAO KUJADILI MWENENDO WA UWEKEZAJI

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Leo Septemba 15, 2023, kumefanyika kikao baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na wataalamu kutoka taasisi zinazojihusisha na uwekezaji hapa Nchini, chenye lengo la kufanya majadiliano juu ya mwongozo na mwenendo wa uwekezaji ndani ya wilaya ya Temeke.

Kikao hicho kimepokea mawasilisho, kimejadili fursa za uwekezaji, pamoja na changamoto mbalimbali zinazowapata wadau wa wawekezaji wilayani humo.

Akizungumza mara baada ya kikao hicho, Bi. Janeth Robert Mtaalamu kutoka taasisi ya Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA) amesema kuwa kikao hiki kimekuwa muhimu kwa manufaa ya uwekezaji Nchini, hasa wilayani Temeke.

"Kwa sisi TCCIA, wawekezaji ni wanachama wetu kwa hiyo tunafurahi kwa hili tukio, na tutakuwa pamoja katika maswala ya uwekezaji ikiwemo utatuzi wa changamoto" alisema

Nae Meneja wa kanda ya mashariki, Kituo Cha Uwekezaji (TIC) Ndg. Fidelis Rubanga amesema kuwa wanatarajia kuandaa makongamano pamoja na wawekezaji kwa ajili ya kujadili mengi katika uwekezaji ikiwemo utatuzi wa changamoto.

Kikao hicho kimefanyika katika ukumbi wa elimu Sekondari uliopo Manispaa ya Temeke.




# MHE.MATINYI ASHIRIKI UZINDUZI WA HUDUMA YA "CHOO SALAMA" KWA WANAFUNZI WA KIKE

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Katika kuhakikisha wanafunzi wa kike wanakuwa safi na salama, Mkuu wa wilaya ya Temeke Mheshimiwa Mobhare Matinyi ameungana na Asasi ya wenza wa viongozi Nchini iitwayo Ladies of New Millenium kuzindua mradi wa choo kwa ajili ya kusaidia watoto wa kike kujisitiri na kupata huduma zote wanazozihitaji wakiwa kwenye hedhi.

Uzinduzi huo uliofanywa na mlezi wa asasi hiyo, Mke wa Waziri mkuu Mama Mary Majaliwa, ulifanyika katika shule ya msingi Mtoni wilayani Temeke.

Choo hicho ambacho kimefanyiwa ukarabati na Asasi hiyo ikiongozwa na mwenyekiti wake mke wa Waziri mkuu mstaafu wa awamu ya nne mama Tunu Pinda, kimewekewa huduma zote muhimu zinazohitajika wakati wa hedhi ikiwemo taulo za kike.

Mhe.Matinyi ametoa shukrani zake za dhati kwa Asasi hiyo kuwezesha upatikanaji wa huduma hiyo hapo shuleni, pamoja na kwa wadau mbalimbali akiwemo Bi Selina Retala, Mkurugenzi mkuu wa HQ Pads kwa kuchangia katoni 100 za taulo za kike kwa ajili ya watoto kujihifadhi wakati wa hedhi.

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo Ndugu Victor Kangati ameishukuru Asasi ya Ladies of New Millennium kwa kuleta mradi huu ambao utasaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi wa kike pindi wanapoingia kwenye hedhi.

Hii ni moja ya jitihada zinazofanywa na viongozi mbalimbali akiwemo mkuu wa wilaya ya Temeke kuhakikisha wanamsaidia Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu kumlinda mtoto wa kike na kumfanya awe katika Mazingira mazuri yatakayomuwezesha kupata elimu bila changamoto zozote.



# RC CHALAMILA AFURAHISHWA NA USHIRIKISHWAJI WA VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI SABASABA.

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam mheshimiwa Albert Chalamila leo Julai 11,2023 ametembelea Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ambapo ameonesha kufurahishwa na ushiriki wa vikundi vya Wajasiriamali.

Mhe.Chalamila amesema Maonesho haya yamebeba taswira ya kitaifa na Kimataifa kwa kuwezesha nchi mbalimbali kushiriki lakini si wafanyabiashara wakubwa tu pia wale wadogo na kati.

Amesema Serikali kupitia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri nchini,imesaidia kwa kiasi kikubwa vikundi hivyo vya ujasiriamali kushiriki Maonesho hayo makubwa.

"Hii ndio dhana ya Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu hii mikopo,na wajasiriamali hawa wamekuwa mashaidi wazuri juu ya mitaji hii ilivyoweza kusaidia kukuza Biashara zao".Alisema Mhe.Chalamila

Akiwa katika viwanja hivyo vya maonesho vya Sabasaba mkuu huyo wa Mkoa ametembelea mabanda ya manispaa ya Temeke,Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi(WCF),SIDO,Wizara ya Kilimo,Benki ya Watu wa Wazanzibar(PBZ) na banda la wa China(China Pavilion).

Maonesho hayo makubwa ya Kimataifa ya Biashara yameanza rasmi Juni 28,2023 na yanatarajiwa kukamilika Julai 13 ambapo nchi mbalimbali zinashiriki.



# UWEKEZAJI BANDARI YA DAR ES SALAAM KUNUFAISHA WENYE BANDARI KAVU (ICD)

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Mkuu wa Wilaya ya Temeke. Mheshimiwa Mobhare Matinyi, tarehe 03/08/2023 alifanya ziara ya kukagua shehena inayohudumiwa na bandari kavu (Inland Container Depot - ICD) ya Harpended Explorer Scout Unit (HESU) iliyopo katika kata ya Miburani, wilayani Temeke.

Katika ziara hiyo aliambatana na mbunge wa jimbo la Temeke Mhe. Dorothy Kilave, Katibu Tawala wa Wilaya ya Temeke Nicodemas Tambo, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Temeke, George Sayi, pamoja na Mwenyekiti wa Mtaa wa Miburani, Abeid Mvuma.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkuu huyo wa Wilaya alisisitiza ushirikiano baina ya serikali na wawekezaji kwani uwekezaji unaotarajiwa kufanywa utaboresha zaidi bandari ya Dar es salaam na kuiwezesha kuhudumia takribani tani milioni 38 za mizigo ifikapo mwaka 2030.

"Ubora wa huduma ya bandari hii umetokana na uamuzi wa Mh. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kununua mitambo mitatu ya kupakua na kupakia makasha ya mizigo (Ship to Shore Gantry - SSG) ambapo mmoja una thamani ya shilingi za Tanzania bilioni 40 hadi 50.

Mhe. Matinyi alieleza kuwa uwekezaji huu utasaidia kuhudumia nchi jirani kwa ukamilifu akizitaja Uganda, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi, Zambia, Malawi, Zimbabwe na hivi sasa hata Msumbiji, Komoro isiyokuwa na bandari kubwa na Sudan Kusini. Mhe. Matinyi alisema nchi hizo kwa mwaka zina shehena ya jumla ya zaidi ya tani milioni 70. Hivi sasa sehemu ya shehena hii inahudumiwa na bandari za Mombasa, Beira, Maputo, Walvis Bay na Durban.

Kati ya tani milioni 21.27 ambazo bandari ya Dar es Salaam ilizihudumia mwaka 2022/23 ni tani milioni 8.5 tu ndizo zilizotoka katika nchi hizi.

"Mipango ya baadaye ya bandari ni kuboresha magati namba 8 hadi 11; kuhamisha kituo cha kupokelea mafuta na gesi kutoka Kurasini kwenda Kigamboni pamoja na kuongeza magati namba 12 hadi 15.

Awali serikali ilishatumia jumla ya dola za Marekani milioni 420 kujenga yadi namba 5 hadi 7 zenye uwezo wa kutunza makasha 10,000; kutanua na kuongeza kina cha mlango bahari wa kuingilia bandarini, kujenga gati namba 0 lenye urefu wa mita 320 na eneo la kutunza magari 6,000; kuongeza kina cha magati namba 1 hadi 7 kutoka mita 7 hadi 14.5 pamoja na upana wake kwa mita 15.

Mhe.Matinyi amefanya ziara hii ikiwa ni moja kati ya malengo yake ya kutembelea maeneo yote yanayojishughulisha na shughuli za kiuchumi wilayani Temeke.




# MKURUGENZI MABELYA: FUATENI SHERIA NA TARATIBU,SERIKALI ITAWAUNGA MKONO

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Ndugu Elihuruma Mabelya pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Mipangomiji ya Baraza la Madiwani na wataalam wa Manispaa ya Temeke, leo hii 03 Agosti 2023 wamefanya ziara ya kutembelea viwanda na vituo vya mafuta , yenye lengo la kuona shughuli za uzalishaji, usalama wa wafanyakazi, ukaguzi wa vibali vya uendeshaji, nyaraka za malipo ya Serikali na kusikiliza changamoto zinazowakabili pamoja na kutoa elimu juu ya usafi wa mazingira.

Miongoni mwa viwanda vilivyotembelewa ni kiwanda cha Polyback Ltd kilichopo Kata ya Mbagala kinachojihusisha na utengenezaji wa mifuko ya plastick, chenye idadi ya wafanyakazi takribani 700.

Akizungumza kwenye ziara hiyo Mkurugenzi Mabelya amepongeza uwekezaji mkubwa unaofanywa nchini na kusisitiza mshikamano baina ya Serikali na wawekezaji.

"Sera ya Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha viwanda vinafanya kazi havifi hivyo, fanyeni biashara na fuateni Sheria,Kanuni,taratibu na miongozo ya uwekezaji na Halmashauri itawaunga mkono".Alisema Mkurugenzi huyo

Wajumbe wa Kamati hiyo pia wamekagua vibali mbalimbali na kutaka wawekezaji hao kuwa wawazi endapo watabaini changamoto yoyote itakayo athiri utendaji wao.

Kwa upande wake mwenyekiti wa Kamati ya mipangomiji Mhe. Juma Mkenga ambaye pia ni diwani wa Kata ya Miburani amepongeza uwekezaji huo wa viwanda kwa kuwa utasaidia kuongeza fursa za ajira kwa watanzania.

Manispaa ya Temeke ni moja ya Manispaa nchini ambazo zinategemea viwanda katika kukuza mapato yake na kutekeleza miradi ya maendeleo.





# ZOEZI LA UPANDAJI MITI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg.Elihuruma Mabelya akishiriki katika zoezi la upandaji miti lilioandaliwa na taasisi ya Aga khan foundation.

Zoezi hilo limefaanyika katika shule ya Msingi Kibasila Manispaa ya Temeke.







Mstahiki wa Meya wa Manispaa ya Temeke Mh.Abdalla Mtinika akikagua timu za Kauzu Fc pamoja na Temeke Manispaa katika hatua ya 16 Bora ya Mashindano ya Ndondo Cup 2023 Mchezo uliofanyika katika uwanja wa Bandari



# DC MOBHARE AAHIDI UWAZI NA HAKI UGAWAJI WA MAENEO SOKO LA ZAKHEM.

**Na** Sweetbetter Njige -TMC Habari

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mobhare Matinyi ametembelea soko jipya la kisasa lililopo Mbagala Zakhem na kuwaeleza Wananchi nia ya Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kutekeleza miradi inayowezesha urahisishaji wa huduma za kijamii kwa Wananchi na kuwa ugawaji wa vizimba na fremu katika soko hilo utazingatia uwazi na haki.

Akieleza umuhimu wa soko hilo kwa jamii Mhe. Mobhare alisema mheshimiwa. Rais amewezesha ujenzi huo ili Wafanyabiashara wanufaike na Jamii ipate huduma katika mazingira sahihi. Alisema

"Rais alitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hapa Mbagala, hii ni kwasababu anajali umuhimu wa huduma za kijamii, tumepata soko la kisasa, litakalochukua Wafanyabiashara wengi zaidi ya waliokuwepo, awali walikua wakifanya biashara zao katika vibanda bila huduma muhimu zozote, hapa zimejengwa fremu za kisasa 150, vizimba vya kisasa 160 na huduma nyingine muhimu, kwa maana hiyo soko hili sio tu limeongeza ubora lakini limeongeza idadi ya Wafanyabiashara"

Aidha Mhe. Mobhare amewatoa hofu Wananchi juu ya utaratibu ugawaji wa vizimba na fremu katika soko hilo kuwa utakua wa haki na uwazi. Alisema

"Niwahakikishie wafanyabiashara mliokuwepo kwenye soko la awali kwamba wote mtarejea hapa na mtapewa sehemu za biashara zenu, na wale walioomba utafanyika utaratibu mzuri na wa haki katika kutoa maeneo yaliyobaki"

Akieleza hali ya ujenzi na maombi ya Wafanyabiashara kuingia katika soko hilo mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amesema

"Ujenzi umekamilika kwa 99.9% kilichobaki ni makabidhiano tu, baada ya kutangaza, mpaka sasa maombi yaliyotufikia ni 3,800, tutaendelea kusimamia na kuhakikisha miundombinu inatunzwa ili Wananchi waendelee kunufaika na Serikali iweze kupata mapato"

Manispaa ya Temeke inaendelea kuwajibika katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali ya Awamu ya Sita kutoa huduma bora za kijamii kwa Wananchi kwa maendeleo endelevu na ustawi wa Taifa.



# "KUHESHIMU NA KUTHAMINI WAZEE NI UTAMADUNI WETU" DC MATINYI

**Na** Sweetbetter Njige -TMC Habari

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mobhare Matinyi amekutana na wazee wanaounda baraza la wazee la wilaya hii katika ukumbi wa Idd Nyundo, manispaa ya Temeke.

Akizungumza wakati wa hotuba yake Mhe. Matinyi amewashukuru wazee hao kwa kufika kwa wingi na kuwahakikishia ushirikiano katika utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Kuheshimu na kuthamini wazee ni utamaduni wetu sisi kama Watanzania, napenda kuwajulisha wazee wangu, nyinyi ni watu muhimu sana kwenye hili Taifa, mnaijua Temeke vizuri, sisi kama Viongozi kama ilivyo utamaduni tutaendelea kuwakimbilia, linapotokea lolote ofisi ya mkuu wa Wilaya,ofisi ya katibu tawala ipo wazi muda wote, tutaendelea kushirikiana kwa karibu"

Aidha Mhe. Matinyi amewasihi wazee hao kuhakikisha wanakua na bima ya afya ya jamii ili kuepukana na usumbufu wakati wa kutafuta matibabu.

Kwa upande wake mwenyekiti wa wazee wilaya ya Temeke ndugu Mohamed Mbonde kwa niaba ya baraza la wazee, amempongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua na kumuamini Mhe. Matinyi,huku akimuahidi ushirikiano. Alisema

"Nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania daktari Samia Suluhu Hassan kwa kukuteua wewe (Mobhare Holmes Matinyi) kuwa mkuu wa wilaya ya Temeke, naomba wazee wenzangu tumpokee,tumpe ushirikiano kama tulivyowapa ushirikiano wakuu wa wilaya wote".

Mkuu wa wilaya ya Temeke anaendelea kukutana na makundi mbalimbali katika jamii kuzungumza nao ili kujua changamoto na namna sahihi za kuziendea.



# TEMEKE YAENDELEA KUTEKELEZA ZOEZI LA SIKU YA LISHE YA MTAA/KIJIJI

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke leo Septemba 15, 2023 imeendesha mafunzo ya siku moja kwa watendaji wa kata zote 23 yanayolenga kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa siku ya lishe ya mtaa/kijiji (SALIKI) ndani ya halmashauri hiyo.

Miongoni mwa mafunzo waliyopatiwa watendaji hao ni pamoja na maandalizi ikiwemo huduma mbalimbali zinazotakiwa kutolewa siku ya lishe pamoja na ujumuishwaji wa wadau waliopo katika maeneo yao ili kufanikisha Siku hiyo muhimu.

Akifungua mafunzo hayo Mganga Mkuu Wilaya Daktari Jonas Lulandala amewataka watendaji kuendelea kutoa ushirikiano kwenye utekelezaji wa shughuli za lishe pamoja na kuheshimu matumizi ya fedha za lishe ili kuikomboa jamii yetu na kuaandaa taifa ambalo ni bora.

Halikadhalika Afisa Lishe Manispaa ya Temeke, Bi. Happy Mkunda ameelimisha kuwa siku hiyo hufanyika mara 4 kwa mwaka katika ngazi ya kijiji au mtaa huku malengo makubwa yakiwa ni kuelimishana maswala ya afya na lishe na kuimarisha upatikanaji wa huduma endelevu kwa mama, mtoto na jamii kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa siku hiyo (SALIKI) ni afua mojawapo inayoweza kuchangia kupunguzwa kwa matatizo ya lishe duni katika jamii, na walengwa wa huduma za Saliki ni watoto wote chini ya miaka mitano , mama wajawazito, mama anaenyonyesha, walezi wa watoto chini ya miaka mitano, wanaume, vijana balehe na jamii kwa ujumla.



# BARAZA LA MADIWANI LAPOKEA TAARIFA ZA HESABU ZA MWISHO KWA MWAKA WA FEDHA2022/2023

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Mhe Arnold Peter leo Agosti 30, 2023 ameongoza kikao cha Baraza la madiwani chenye lengo la kupokea na kujadili taarifa ya hesabu za mwisho za halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulioishia Tarehe 30 Juni 2023.

Akiwasilisha taarifa hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi, Mwekahazina wa Manispaa CPA Charles O Ondiek amesema kuwa halmashauri kwa mwaka huo wa fedha imefanikiwa kukusanya na kupokea jumla ya kiasi Tshs Bilioni 149, ambapo kati ya hizo Bilioni 43 ni fedha kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani, Huku Bilioni 79 ikiwa ni ruzuku ya matumizi ya kawaida na Bilioni 37 ni ruzuku ya miradi ya maendeleo.

Vilevile Bilioni 138 zimetumika katika shughuli mbalimbali za halmashauri ikiwa ni sawa na 95% ya makisio ya bajeti kwa mwaka huo wa fedha.

Halkadhalika amebainisha kuwa kwa mwaka huo wa fedha halmashauri imepata ongezeko la Bilioni 1.6 kwenye bakaa ya fedha katika akaunti zote za halmashauri ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita yaani 2021/2022.

Ameongeza kuwa kutokana na ongezeko la miradi ya ujenzi, halmashauri imepata ongezeko la thamani ya mali halisi za kudumu kwa Tshs Bilioni 4.8 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita.

Kwa upande wao waheshimiwa madiwani wamepongeza maandalizi na uwasilishwaji wa taarifa




# DC MATINYI AFUNGUA KONGAMANO LA MAADILI KWA WATOTO

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Leo Agosti 7, 2023, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Mobhare Matinyi, ameshiriki kufungua kongamano la mafunzo ya maadili kwa watoto wa shule za msingi lililoandaliwa na asasi ya wenza wa viongozi nchini iitwayo Ladies of New Millenium.

Kongamano hilo lililowakusanya wanafunzi 800 wa darasa la sita na saba limefanyika katika ukumbi uliopo viwanja vya Sabasaba, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mhe. Matinyi aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo amewataka watoto kuzingatia elimu, michezo, kuepuka vishawishi, kuwasiliana kwa karibu na walimu wao na wazazi pindi wanapokumbana na vitendo vya kikatili au vilivyo kinyume na maadili.

Mhe. Matinyi pia aliwataka watoto wa kiume kutojihusisha na uhalifu kwa kuwa serikali inafanya juhudi kubwa kuhakikisha watoto wote wanapata elimu.

"Kazi yenu kubwa ni kuwa wanafunzi bora, epukeni vishawishi, msiharakishe kwenda kwenye utu uzima huu ni wakati wa kwenda shule," alisisitiza Mhe. Matinyi na kuongeza kuwa juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutoa elimu bure, kujenga madarasa na shule zinapaswa kuthaminiwa kwa watoto kusoma kwa bidii ili kujenga taifa la kesho.

Kongamano hilo limehudhuriwa na wanafunzi wa shule za Msingi Bokorani, Mtoni, Mtoni Sabasaba, Lioness Miburani, Umoja, Twiga, Sokoine na Moringe.




# MHE.MTINIKA AWATAKA WANANCHI KUCHANGAMKIA FURSA MAONESHO YA SABASABA

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika amewataka wananchi na hasa wakazi wa Manispaa hii kuchangamkia fursa za kibiashara katika Maonesho ya Biashara Kimataifa(Sabasaba).

Ametoa wito huo leo Julai 8,2023 alipotembelea Maonesho hayo yalioanza rasmi Juni 28 mwaka huu.

Mhe.Mtinika amesema wananchi hawana budi kuyatumia Maonesho hayo kutangaza bidhaa zao kwa kuwa yana tija ukizingatia uwepo wa nchi nyingi zinazoshiriki maonesho haya ya Biashara ya Kimataifa.

"Sisi kama viongozi tumefurahishwa na mabadiliko makubwa yaliyofanyika mwaka huu na ni wakati muafaka sasa kwa wakazi wa Temeke kuchangamkia fursa zinazopatikana katika Maonesho haya".Alisema Mstahiki meya Mtinika

Akiwa katika Banda la Manispaa ya Temeke,Meya Mtinika ameeleza kufurahishwa kwake na jinsi mikopo ya asilimia 10 ilivyoweza kunufaisha vikundi vya wajasiriamali mbalimbali.

Katika ziara hiyo Mstahiki meya Mtinika aliambatana na Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya ambapo kwa pamoja walitembelea baadhi ya mabanda yakiwemo la Wizara ya Ardhi,Wizara ya Kilimo na la Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi(WCF)



# MICHEZO IENDANE NA UZALENDO -DC MATINYI

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Mobhare Matinyi, leo Agosti 27, 2023 amekipongeza Chama cha Mbio za Mwendo wa Pole-pole (Temeke Jogging Association- TEJA), kwa kuandaa tamasha kubwa lililojumuisha mikoa yote ya Zanzibar na mikoa 12 ya Tanzania Bara.

Mhe Matinyi aliyekuwa akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Mhe. Albert Chalamila ame-pongeza uzalendo ulioone-shwa na chama hicho kwa kuandaa zoezi la upimaji afya pamoja na uchangiaji damu kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Temeke sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu ya kupiga vita ukatili wa kijin-sia kwa watoto na wana-wake na kupinga mahusia-no ya jinsia moja.

"pamoja na uanamichezo lakini mmejali pia wahitaji na hii ndivyo inavyotakiwa Michezo iendane na uzalen-do"

Kabla ya kugawa vyeti kwa wadhamini na washiriki, Mhe. Matinyi amewasilisha salamu za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aki-wapongeza washiriki wa 'jogging' hiyo kwa kujali afya zao kupitia mazoezi, kuchangia damu na kupin-ga unyanyasaji wa kijinsia.

"Mhe. Mkuu wa Mkoa ame-nituma niwasilishe salamu za Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kiongozi mwanamichezo, kwenu nyote washiriki " alisema Mhe. Matinyi.

Katika risala yao, TEJA kwa niaba ya mamia ya wakim-biaji, wamemwomba Rais ashiriki nao katika mbio hizo za mwendo wa pole pole katika siku za usoni.

Aidha, Mhe. Matinyi pia amewasilisha pongezi na shukrani kutoka kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa wanamichezo hao kuchangia damu; Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Pindi Chana, kwa wananchi hao kujali michezo; na pia kutoka kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dor-othy Gwajima, kwa washiri-ki hao kuunga mkono juhudi za serikali kupiga vita unyanyasaji kwa watoto na wanawake.

Tamasha hilo la mbio za mwendo wa polepole wa umbali wa kilomita sita limefanyika kuanzia Kigam-boni kwenye daraja la Mwl.-Julius Nyerere hadi Uwanja wa Uhuru, likiongozwa na Mhe. Matinyi pamoja na Mwenyekiti wa chama hicho Mhandisi Rashid Pazi na Makamu wake Janet Maseke.




# DC MATINYI AZINDUA RASMI ZOEZI LA ARDHI CLINIC (HATI PAPOHAPO)

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Mkuu wa wilaya ya Temeke Mheshimiwa Mobhare Matinyi ametoa wito kwa wakazi wa Temeke kujitokeza kwa wingi kwa ajili kuboresha usalama wa milki za ardhi zao ikiwemo kugawiwa hati papo hapo.

Mhe. Matinyi ameyasema hayo leo Septemba 20, 2023 kwenye mkutano wa uzinduzi wa Ardhi Clinic, zoezi ambalo lipo chini ya Mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi (LTIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi.

Mhe. Matinyi amemshukuru Mhe. Rais Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha milki za ardhi nchini na kuwataka Wananchi kutumia fursa hiyo muhimu.

"Mheshimiwa Rais ametafuta fedha kwa ajili ya kuboresha milki za ardhi kwenye maeneo yetu, hivyo Wananchi tutambue umuhimu na tujitokeze kwa wingi, jambo zuri huduma zote zinatolewa kielektronikia unapewa hati yako na rekodi zako zinahifadhiwa kidigitali " alisema DC Matinyi

Kwa upande wake mwakilishi wa mradi Bi. Aisha Masanja amesema kuwa zoezi hilo litadumu kwa siku 25 na litapita kwenye mitaa mitano.
"Tumeanzia hapa Mbagala kuu mashariki, na tutakuwa hapa viwanja vya Zakhiem kuwahudumia wananchi kwa muda wa siku tano, na baada ya hapo zoezi hili litahamia kwenye mitaa mingine ambayo ni Buza, kisewe, Mwembebamia,na Mianzini" alisema Bi. Aisha

Mara baada ya Mkuu wa wilaya kuzindua rasmi zoezi hilo, alikabidhi kwa Wananchi hati miliki zilizoshughulikiwa papo hapo.

Mradi wa uboreshaji usalama wa Milki za ardhi (LTIP) unalenga kutatua changamoto zote zinazokabili urasimishaji ardhi nchini ikiwemo kupanga na kupima maeneo yanayoyohitaji leseni za makazi na hati Miliki, kurahisisha gharama za upimaji, kutoa hati na leseni za makazi pamoja na kuboresha miundo mbinu ya ardhi kwa nchi nzima.












PICHA: Matukio mbalimbali wakati wa Mbio maalum za hisani zilizoandaliwa na Benki ya CRDB "CRDB BANK MARATHON" .

Mbio hizo zenye lengo la kutekeleza sera ya Benki hiyo ya kusaidia Jamii katika ambapo kila mwaka hutenga asilimia moja kutoka kwenye faida inayopata na kuipeleka kwenye Jamii kusaidia masuala mbalimbali ikiwemo Afya,elimu,maji nk.

Mgeni rasmi kwenye Mbio hizo zilizoanzia viwanja vya Green Ground Oystebay asubuhi ya leo Agosti 13,2023 alikuwa ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt.Hussein Mwinyi.



# KAMPENI YA USAFI TEMEKE YAVUTIA WADAU

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Jitihada za viongozi wa wilaya ya Temeke katika kampeni za usafi zinazofanyika mara kwa mara zimewagusa wadau mbalimbali na hatimaye kuiunga mkono Temeke katika kampeni hizo.

Akizungumza katika zoezi la usafi lililofanyika leo tarehe 30 Septemba, 2023, kwenye kata ya Miburani eneo la Temeke mwisho, Mkuu wa Wilaya Mhe. Mobhare Matinyi amesema kwamba karibu kata zote 23 za wilaya hiyo zimepata wageni rasmi kutoka kada na sehemu mbalimbali.

Mhe. Matinyi aliongeza zaidi kuwa kwa kuvutiwa na usafi wa mazingira wilayani humo, kampuni ya fedha ya Bayport imetoa miche ya miti 500 iliyopandwa tarehe 29 Septemba, 2023 wilayani humo wakati wa kuhitimisha awamu ya kwanza ya usafi ya mitaro na mifereji.

Mhe. Matinyi aliongeza zaidi: "Wakati tunazindua wiki ya kusafisha mitaro na mifereji, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayesimamia Muungano na Mazingira, Dkt. Selemani Jaffo, alikuja kutuunga mkono kwa sababu aliona tunafanya jambo jema na wana Temeke tuna mwamko."

Kabla ya hapo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila, alikuwa mgeni rasmi kwenye siku ya usafi duniani wilayani humo ambamo iliadhimishwa kwa kufanya usafi kwa wiki nzima huku akitoa wito kwa wengine kuiiga Temeke.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Miburani Bw. Ali Kiaka ametoa rai kwa wananchi wa maeneo hayo kuendelea kutunza mazingira na kuacha tabia ya kutupa taka kwenye mitaro na mifereji.



# DC TEMEKE AKABIDHI BENDERA KWA VIJANA WANAOTEMBEA NCHI NZIMA

**Na** Shalua Mpanda -TMC Habari

Mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe. Mobhare Matinyi leo Agosti 15, 2023 amewakabidhi bendera ya Taifa vijana saba wazalendo wa Temeke wanaoanza matembezi kuzunguka mikoa 16 ya Tanzania bara kwa lengo la kuhamasisha vijana kufanya kazi.

Tukio hilo limefanyika katika ofisi za mkuu wa wilaya na kushuhudiwa na Mstahiki Meya wa manispaa ya Temeke Mhe.Abdallah Mtinika na Katibu Tawala wa wilaya hii Bw.Nicodemas Tambo.

Akizungumza katika tukio hilo Mhe Matinyi amepongeza uamuzi wa kishujaa na kizalendo wa vijana hao kwa kuzitangaza juhudi zinazofanywa na Mhe.Rais Dkt Samia Suluhu Hassan zinazopaswa kuungwa mkono na vijana wengine.

Aidha amewataka vijana hao kutangaza maendeleo yaliyoletwa na Serikali ya awamu ya sita katika wilaya ya Temeke.

"Kwa mfano katika sekta ya elimu sekondari, kwa mwaka wa fedha uliopita Mheshimiwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ametuletea Bilioni 10, Kwa hiyo mnatakiwa mkatangaze haya huko mnapopita ili watu wafahamu Serikali inachofanya". Alisema Mkuu huyo wa Wilaya

Kwa upande wake Mstahiki meya Abdallah Mtinika amewatia moyo vijana hao kwa kuutumia ujana wao na kuhimiza uzalendo, ushupavu, kuitetea Nchi, na kuacha alama katika maisha ya vijana wengine.

Vijana hao wanatarajia kutembea zaidi ya kilometa 3000 katika mikoa hiyo 16 huku matembezi hayo yakitarajiwa kufikia tamati Oktoba 14 mwaka huu katika kilele cha Mbio za Mwenge



# WAZIRI SHAMATA ATEMBELEA BANDA LA TEMEKE MAONESHO YA NANENANE

**Na** Sweetbetter Njige -TMC Habari

Leo Agosti 03,2023 Waziri wa kilimo,umwagiliaji,maliasili na mifugo Zanzibar mheshimiwa Shamata Shaame Khamis ameambatana na mwenyeji wake mkuu wa mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima kutembelea banda la manispaa ya Temeke wakati wa ukaguzi wa mabanda ya washiriki wa maonesho ya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) katika viwanja vya Mwl. J.K Nyerere na kufurahishwa na mambo mbalimbali yaliyopo bandani hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari Waziri Shamata amesema amefurahishwa na ushiriki wa manispaa ya Temeke na kutumia nafasi hiyo kuwasihi Wananchi kushiriki kikamilifu kujenga uchumi wa Taifa kupitia uzalishaji wa mazao ya chakula na ufugaji. Alisema "Nimefurahi kupata nafasi kufika Temeke, tunathamini sana jitihada mnazofanya na tunawasihi muongeze ufanisi katika kujenga uchumi wa Dar as Salaam na Nchi nzima kwa ujumla, kwa kuongeza uzalishaji wenye tija"

Aidha Waziri Shamata ameeleza nia ya dhati ya Serikali zote mbili (Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar) kuwekeza nguvu kubwa katika kilimo na ufugaji. Alieleza

"Kuzalisha kwa wingi kunasaidia kulinda amani ya Nchi, tujifunze kwa mengi yanayojitokeza katika Dunia kutokana na matishio ya njaa, kuna Nchi zimekosa amani kwasababu ya njaa, hivyo kazi yote inayofanyika hapa inalenga kutuliza na kuchochea amani ya Nchi, ni wajibu wetu kuongeza ufanisi katika uzalishaji ambao pia utasaidia kupunguza mfumuko wa bei"

Kwa upande wake mkuu wa mkoa wa Morogoro Mhe. Malima amemshukuru Mhe. Shamata kwa ziara yake na kueleza nia ya mkoa wa Morogoro na mikoa jirani kujifunza kutoka Zanzibar.

"Tumefarijika sana kukukaribisha Morogoro, uwepo wako umethibitisha undugu wetu,historia yetu na umoja wetu, kule Zanzibar kuna kilimo cha kimkakati cha karafuu, tunajipanga kuja kujifunza kuzalisha karafuu kwakua kuna misingi iliyoboreshwa kimasoko, tunataka kuanza kuzalisha karafuu kwa kufuata vigezo vinavyohitajika katika soko la Kimataifa na Zanzibar mnajulikana kwa hilo"

Manispaa ya Temeke inashiriki katika maonesho hayo ya Wakulima na Wafugaji na inawakaribisha Wananchi wote kufika bandani hapo ili kujifunza juu ya masuala mbalimbali yahusuyo kilimo ma ufugaji wa kisasa.



# MSTAHIKI MEYA AHIMIZA ULIPAJI NA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MAENDELEO YA TEMEKE

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Mheshimiwa Abdallah Mtinika ametoa wito kwa wananchi kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi na ushuru stahiki ili kuwezesha Manispaa na Serikali kwa ujumla kupata mapato kwa ajili ya kupanga mikakati ya kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Meya ametoa wito huo leo Septemba 27, 2023 kwenye mkutano na waandishi wa habari kuelezea mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulioishia tarehe 30 Juni 2023.

Mhe. Mtinika amesema kuwa Halmashauri kwa mwaka huo wa fedha imefanikiwa kukusanya Tshs Bilioni 43.9 kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ya ndani ikiwa sawa na asilimia 101 ya lengo la makusanyo na Tshs Bilioni 19.9 kutoka humo zimetumika kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwa mwaka huu mpya wa fedha 2023/2024 kiasi kilichopangwa kukusanywa ni Tshs Bilioni 47.7, hivyo niwaombe wananchi tulipe kodi, wenye malimbikizo ya madeni walipe lakini pia tumejipanga kudhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato ikiwemo kupokea taarifa ya vyanzo vinavyopotea ili kuzuia uvujaji wa fedha za halmashauri" alisema Mhe. Mtinika.

Vilevile ameeleza kuwa halmashauri ilipokea ruzuku kutoka serikali kuu ya Tshs Bilioni 10.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa shule mpya za msingi na sekondari, ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na uboreshaji katika sekta ya afya.

Halikadhalika ameeleza kuwa halmashauri ilifanikiwa kutenga asilimia kumi ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya utoaji mikopo kwa wanawake , vijana na walemavu ambapo kiasi cha Tshs Bilioni 2.9 kimetumika kwa makundi hayo.

Amehitimisha mkutano huo kwa kusisitiza wananchi kuendelea kutunza amani iliyopo nchini na kuishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na Menejimenti na watendaji wote wa Halmashauri ya Temeke kwa kuwezesha mafanikio hayo.




# TEMEKE YAPANDA MITI 500

**Na** Sweetbetter Njige -TMC Habari

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mhe. Mobhare Matinyi, leo Septemba 29, 2023, ameongoza wananchi katika zoezi la upandaji miti 500 pembezoni mwa barabara katika kata za Buza na Makangarawe.

Miti hiyo imetolewa na kampuni ya fedha nchini ya Bayport Tanzania inayotaka kupanda miti milioni moja nchini kote.

"Leo tunapanda miti 500 na tutakuwa na kazi ya kuitunza lakini wenzetu Bayport wamesema watatusaidia kwa siku 60 na baadaye tuitunze wenyewe na tubadili mtazamo wetu kuhusu usafi na mazingira," alisema Mhe. Matinyi na kuishukuru Bayport.

Awali kabla ya tukio hilo lililohudhuriwa pia na Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg. Elihuruma Mabelya na Diwani wa kata ya Buza, Mhe. James Mkude, Mhe. Matinyi aliwaongoza wananchi kufanya usafi katika mitaro na mifereji huku akisisitiza kuwa hii ni awamu ya kwanza ya kujiandaa na mvua za El Nino.

Wilaya ya Temeke itafunga mwezi tarehe 30 Septemba kwa kufanya usafi katika kata zote 23 kila moja ikiwa na mgeni wake rasmi.






# TEMEKE WAJIANDAA KUKABILIANA NA MVUA ZA EL-NINO

**Na** Shalua Mpanda

Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amefanya ziara ya kukagua usafishaji wa mfereji mkubwa wa Serengeti katika kujiandaa kukabiliana na uwezekano wa mvua za El-nino zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Akiwa katika eneo la Keko ambapo aliongozana na diwani wa Kata hiyo mheshimiwa Jasdeep Bahbra,Mkurugenzi Mabelya amesema wameamua kuanza kusafisha mitaro na mifereji yote katika Halmashauri hii kwa lengo la kuokoa na kupunguza maafa yanayoweza kujitokeza hapo baadae.

"Tunaelekea kwenye hatari ya mvua hizo,wito wangu kwa wananchi kulinda mitaro hii maana madhara yake ni mafuriko ambayo yatahatarisha maisha ya watu".Alisema Mkurugenzi huyo

Amesema mtaro huo ambao umeigharinu Serikali kiasi cha shilingi bilioni 19 kuujenga,umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mafuriko katika maeneo mengi ndani ya wilaya hii.

Kwa upande wake diwani wa kata ya Keko Mhe.Jasdeep amesema wameandaa zoezi maalum la kuulinda mtaro huo ili kuweza kutunza na kuweza kuwezesha maji kupita kama ilivyokusudiwa.

Mfereji huo unaopita katika kata za Miburani,Sandali pamoja na Keko umekuwa ukichafuliwa na baadhi ya wananchi hali ambayo imekuwa ikisababisha mafuriko ya mara kwa mara katika maeneo hayo.



# MKUU WA WILAYA TEMEKE ATEMBELEA WODI YA WAZAZI TEMEKE

**Na** Joanita Joseph -TMC Habari

Leo Septemba 21, 2023 mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Mobhare Matinyi ameungana na Mbunge wa jimbo la Temeke Mhe.Dorothy Kilave, Viongozi wa Chama (CCM) na wadau mbalimbali wa afya kukabidhi nepi za kisasa (Diapers) kwa Wanawake waliojifungua na wanaotarajia kujifungua katika hospitali ya rufaa ya mkoa Temeke.

Akikabidhi nepi hizo Mhe. Matinyi ameeleza nia ya dhati iliyowasukuma Viongozi hao na wadau wa afya kuungana pamoja kuwapongeza na kuwafariji wazazi waliojifungua katika hospitali hiyo, alisema.

"Tumekuja kuwaona kina mama waliokwisha jifungua, tukaona tusije mkono mtupu tumeleta zawadi ya nepi za kisasa (Diapers) kwa watoto wachanga, hii iwe zawadi kwa kina mama hawa, wanafanya kazi kubwa ya kuleta maendeleo kwa Taifa kwa kuwa wao ndio msingi wa maisha.Alisema Mhe.Matinyi

Aidha Mhe. Matinyi amesema wananchi wa Temeke wanapaswa kujivunia uwepo wa wataalam wenye juhudi na utu wanaohudumia katika hospitali hiyo kwa kuthamini jitihada zao.

"Nitoe shukrani kwa Mganga mfawidhi na timu yako, hospitali yetu inahudumia Wananchi wengi sana, mnafanya kazi kubwa tunapaswa kujivunia uwepo wa wataalam wanaofanya kazi nzuri kwa moyo wa kujitolea ikiwemo kufanya masuala ya uchunguzi". Alisema Mkuu huyo wa Wilaya

Kwa upande wake Mganga mfawidhi wa hospitali hiyo Dkt. Joseph Kimaro amemshukuru mkuu wa Wilaya hii kwa jitihada zake za kufanikisha upatikanaji wa msaada huo na kumuahidi watumishi wa hospitali hiyo wataendelea kutoa huduma kwa upendo na uaminifu.

"Nikushukuru kwa jitihada ulizochukua kufanikisha upatikanaji wa msaada huu utakaowasaidia kina mama waliokwisha jifungua. Hospitali hii inahudumia Wananchi wa Temeke wanaokaribia 1,500,000 lakini inahudumia zaidi ya hao kutoka maeneo jirani, tutaendelea kuwahudumia kwa upendo ili waweze kurudi kulihudumia taifa". Alisema Dkt.Kimaro

Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Temeke ni moja kati ya hospitali inayopokea na kuhudumia wagonjwa wengi nchini.
.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

# TANGAZO KWA UMMA

## KUREJESHWA KWENYE KITUO CHA KAZI CHA AWALI

MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE ANAPENDA KUTOA TAARIFA KUWA MWALIMU **MAGANGA M. JAPHET** MWENYE **CHECK NO.9607099** MWAJIRIWA WA MANISPAA YA TEMEKE MWENYE CHEO CHA **MWALIMU MWANDAMIZI DARAJA A,** ALIOMBA KIBALI CHA KUAZIMWA CHA TAREHE **21 AGOSTI, 2017** NA KUPEWA KIBALI CHA KUAZIMWA NA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) KWA BARUA KUMB NA. **CA.87/164/01/'B'/160** YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS -UTUMISHI.

KIBALI HIKI KILIKUWA CHA MIAKA MITATU KUANZIA **DESEMBA 2017 HADI SEPTEMBA 30, 2020.**

AIDHA MWALIMU MAGANGA ALIOMBA NYONGEZA YA KIBALI KWA BARUA YA **TAREHE 01 JUNI, 2020** NA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS - UTUMISHI ALIMPA KIBALI CHA NYONGEZA KUMB NA **.CA.164/228/01/'V'/68** CHA **TAREHE 10 AGOSTI, 2020** KINACHOISHIA **TAREHE 30 SEPTEMBA, 2023.**

MWALIMU MAGANGA ALIOMBA TENA KIBALI CHA KUAZIMWA KWA MARA YA TATU AMBAPO KATIBU MKUU OFISI YA RAIS - UTUMISHI **HAJARIDHIA** MAOMBI HAYO HIVYO BASI MWALIMU MAGANGA M. JAPHET ANAPASWA KUREJEA KWENYE KITUO CHAKE CHA KAZI MARA MOJA MNAMO TAREHE **01 OKTOBA, 2023.**

IMETOLEWA NA:

**MKURUGENZI MANISPAA YA TEMEKE**
**23.09.2023**

MKURUGENZI WA MANISPAA
TEMEKE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

:

# TANGAZO

MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE ANAWATANGAZIA WAMILIKI WA TAASISI,VIWANDA,MAKAMPUNI,HOTELI,NYUMBA ZA KULALA WAGENI NA WAFANYABIASHARA WOTE NDANI YA MANISPAA AMBAO BADO HAWAJALIPA USHURU WA HUDUMA YAANI SERVICE LEAVY KWA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) KULIPA USHURU HUO.NA WALE WENYE MABANGO KULIPA USHURU WA MABANGO YAO.

KADHALIKA WAFANYABIASHARA AMBAO LESENI ZAO ZIMEKWISHA MUDA WAKE KUHUSISHA LESENI HIZO, AMBAO HAWANA LESENI KUKATA LESENI, AMBAO WAMEPANGA KWENYE VIBANDA VYA MANISPAA NA WANADAIWA KODI YA PANGO KULIPA MADENI YAO, KWANI KINYUME CHAKE WATAONDOLEWA,NA VIBANDA HIVYO WATAPEWA WENGINE.

AIDHA MKURUGENZI ANAWAKUMBUSHA WAKAZI WOTE WA TEMEKE KUWA NI KOSA KISHERIA KUJENGA,KUKARABATI MAJENGO, KUFANYA SHEREHE YOYOTE AU KUTOA MATANGAZO MADOGO MADOGO BILA KUWA NA KIBALI CHA MANISPAA, NA KWAMBA OPERESHENI MAALUM YA MTAA KWA MTAA INAENDELEA,NA HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA WOTE WATAKAOBAINIKA KUFANYA HIVYO.

"LIPA KODI NA USHURU KWA MAENDELEO YA MANISPAA YA TEMEKE".

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI.
**MANISPAA YA TEMEKE.**

92 Barabara ya Mandela / Taifa, S.L.P 46343, Dar es Salaam, Simu +255222928132, Nukushi +255222928137,
Barua Pepe: temeke@temekemc.go.tz , Tovuti: www.temekemc.go.tz

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**
**S. L.P 46343 TEMEKE, DSM.**
**SIMU: +255 22-2928132**
**NUKUSHI: +255 22-2928137**
**BARUA PEPE: temekemc.go.tz**
**TOVUTI: www.temekemc.go.tz**